

SWAUMU ZA SUNNAH.

Mtume swalallahu alayhi wassalaam alipendekeza na kutilia mkazo kufunga siku zifuatazo;

1. Kufunga siku sita za mwezi wa Shawwal kwa kauli yake mtume:

(Mwenye kufunga mwezi wa Ramadhani kisha akafuatisha siku sita za mwezi wa Shawwal atakuwa kana kwamba amefunga mwaka mzima). (Ameipokea Imamu Muslim: 1164).

2. Swaumu ya siku ya jumatatu na Alhamisi.

3. Swaumu ya Siku tatu za kila mwezi akifunga masiku meupe ni bora zaidi nazo ni tarehe 13, 14 na 15 ya kila mwezi kwa kalenda ya Hijriya sio ya miladiya.

4. Kufunga siku ya Ashurah ambayo ni tarehe kumi ya mwezi wa Muharam, na inapendekezwa kufunga siku moja kabla yake au siku moja baada yake kutofautiana na mayahudi.

Mtume (saw) anasema katika hadithi aliyoipokea Abu Qatada (R.A) kuwa: (Swaumu ya siku A'shura natarajia kwa Allah ujira wa malipo ya kufutiwa madhambi ya mwaka uliopita) (Ameipokea Imamu Muslim:1162).

5. Swaumu ya siku ya A'rafa nayo ni siku ya tisa ya mwezi wa Dhul-Hija kwa hadithi ya Mtume (saw) inayosema:

((Swaumu ya siku ya A'rafa natarajia malipo ya kufutiwa madhambi ya mwaka kabla yake na mwaka baada yake)) (Amepokea Imamu Muslim 1162).

SIKU AMBAZO NI HARAMU KUFUNGA.

1. Kufunga siku ya Eid mbili, Eidl fitri na Eidil adh-a.

2. Kufunga siku za Tashriq tatu, tarehe kumi na moja, kumi na mbili na kumi na tatu katika mwezi wa Dhul -Hija, na anajizua na hili kwa mwenye kuhiji kwa nia ya kuunganisha (kati ya Umrah na Hija) au tamatuu ikiwa hajapata kichinjo.

3. Kufunga kwa mwenye hedhi na nifasi.

4. Kufunga sunnah mwanamke na mumewe yupo bila ya idhini yake, kwa kauli ya Mtume (saw) anasema:

(Asifunga mwanamke swaumu ya sunnah na mume wake yupo isipokuwa kwa Idhini yake ila swaumu ya Ramadhan) (Ameipokea Bukhar na Muslim: 5192,1026).